Iwapo umechanganya mbaazi na zao lingine mfano mahindi/mtama, nyunyizia kiuwadudu baada ya kuvuna zao hilo. Wakati wa kuchanganya na kunyunyizia kiuwadudu tumia vifaa kinga kuzuia athari mwilini.

## Jinsi ya kuchangaya viuwadudu

- Changanya 40cc za karate katika lita 15 za maji au 40cc katika ULVA kwa lita moja ya maji au
- Changanya 40cc za Amerate 5EC katika lita 15 za maji au
- Changanya 40cc za Profecron katika lita 15 za maji au
- Changanya 40cc za COLT (chlorpyrifosi) katika lita 15 za maji na kisha nyunyiza shambani.

## JINSI YA KUVUNA

**Mbaazi mbichi**

Vuna wakati vitumba vimeshajaza vizuri.

**Mbaazi kavu**

Vuna wakati mbaazi zimekomaa vizuri, vitumba vinapobadilika kuwa na rangi ya kahawia. Vuna kwa kuchuma vitumba au kwa kukata matawi. Kausha juani, piga na peta. Wadudu waharibifu wa ghalani huanzia mashabulizi shambani kama zao halikuvunwa mapema. Kwa hiyo vuna mbaazi mapema ili kupunguza tatizo hilo.

## KIASI CHA MAVUNO

Mbaazi za muda wa kati hutoa mavuno kiasi cha kilo 3000 kwa aina ya TUMIA, ILONGA -14-M1 kilo 3000 - 3200 na ILONGA - 14-M2 kilo 3000 - 3500. kwa hekta ambayo ni sawa na kilo 1200 - 1400 kwa ekari moja (magunia 12 - 14 kwa ekari). Kiasi cha mavuno ya mbaazi iliyochanganywa na zao lingine itategemea na zao ililopewa kipaumbele wakati wa kupanda.

## KUHIFADHI

Baada ya kupeta, weka mbaazi zako kwenye vyombo safi visivyo na wadudu au;

- Tumia kiuwadudu cha maji cha Actellic 50EC,
- Hifadhi bila kutumia kemikali kwa njia ya mifuko ya PICS.
- Changanya kipaketi cha gramu 200 cha kiuwadudu shumba katika magunia mawili ya kilo mia (100kg) ya mbaazi.

## UPATIKANAJI WA MBEGU

Mbegu za awali za muda wa kati zinapatikana katika Kituo cha Utafiti wa Kilimo Ilonga na mbegu za msingi zinapatikana kwa wakala wa mbegu za kilimo (ASA).

**Kwa maelezo zaidi pamoja na mahitaji ya mbegu wasiliana na:**
Mkurugenzi wa Kanda, Utafiti na Maendeleo Kanda ya Mashariki,
Kituo cha Utafiti wa Kilimo, ILONGA,
Sanduku la Posta 33, Kilosa, Tanzania
Simu: 023 2623201, Fax: 023 2623284
Barua pepe: ilonga.ari@gmail.com

# KILIMO BORA CHA MBAAZI ZA MUDA WA KATI



**Kimetayarishwa na:**
Kituo cha Utafiti wa Kilimo, ILONGA,
Sanduku la Posta 33, Kilosa, Morogoro,
Simu: 023 2623201
Nukushi: 023 2623284
Baruapepe: ilonga.ari@gmail.com

©Chapisho la Utafiti wa Kilimo Kanda ya Mashariki– A R I Ilonga

**TOLEO 2016**
**Uchapishaji umegharamiwa na Mradi wa AGRA**

Scanned with CamScanner

## KILIMO BORA CHA MBAAZI ZA MUDA WA KATI

### UTANGULIZI

Mbaazi ni zao la jamii ya mikunde, faida kubwa za zao hili ni:

- Chanzo cha viini lishe vya protini kwa binadamu na wanyama
- Linavumilia ukame
- Hupunguza umasikini kwani zao hili ni chanzo cha mapato kwa kaya
- Hurutubisha udongo
- Linaweza kuchanganywa na mazao mengine shambani kama vile mahindi na mtama

Ili kujipatia mazao mengi na bora ya mbaazi za muda kati zingatia maelezo yaliyomo kwenye kipeperushi hiki.

### AINA

Mbaazi za muda wa kati zinazopendekezwa ni aina ya TUMIA, ILONGA 14-M1 na ILONGA 14-M2. Mbaazi za muda wa kati zimefanyiwa utafiti na kuonekana ni bora, pamoja na kutoa mazao mengi katika sehemu mbalimbali, TUMIA hukomaa kati ya siku 140 –180, ILONGA 14-M1 hukomaa kati ya siku 145 – 182 na ILONGA 14-M2 hukomaa kati ya siku 142 -185. Mbaazi za muda wa kati zina mbegu nyeupe ambazo zinapendwa na walaji na wafanya biashara. Pia aina hii ina uwezo mzuri wa kutoa machipukizi (ratooning).

### MAENEO YA KUPANDA

Mbaazi za muda wa kati zinafaa kupandwa maeneo ambayo yana joto kiasi. Maeneo hayo ni yale yaliyo kati ya mita 500 hadi 1500 kutoka usawa wa bahari.

Katika maeneo ya chini ya mita 200 kutoka usawa wa bahari ambapo kuna uwezekano wa joto kuzidi panda aina ya mbaazi ya muda mfupi Komboa.

### WAKATI WA KUPANDA

Mbaazi za muda wa kati zipandwe wakati wa masika. Kwa kanda zote zipandwe kuanzia Disemba hadi mwishoni mwa Februari. Mbaazi hizi zinaweza kuchanganywa na mazao mengine kama vile mahindi na mtama. Kama zao la mbaazi litachangaywa na mahindi au mtama, mazao yote yapandwe wakati mmoja. Zao linalochanganywa na mbaazi ni lazima liwe linakomaa kabla ya mbaazi ili kupunguza ushindani kwa virutubisho vilivyomo kwenye udongo na mwanga wa jua kwa mbaazi.

### NAFASI YA KUPANDA NA KIASI CHA MBEGU

#### Mbaazi peke yake

Panda kwa umbali wa sentimita 100 kati ya mistari na sentimita 30 kati ya mashina. Panda mbegu mbili 2 kila shimo. Wiki mbili baada ya kuota, punguza mmea mmoja ili ubaki mmoja kwa kila shimo. Ili kupanda hekta moja unahitaji wastani wa kilo 15 za mbegu ya mbaazi za muda wa kati ambayo ni sawa na kilo 6 kwa ekari.

#### Mseto wa mbaazi na mahindi au mtama wa muda mfupi

Panda mahindi au mtama sentimita 100 kutoka mstari hadi msitari na katikati ya mistari ya mahindi/mtama panda mbaazi. Acha sentimita 30 kutoka shina hadi shina la Mbaazi na sentimita 30 shina hadi shina la mahindi/mtama. Unahitaji wastani wa kilo 6 za mbaazi ili kupanda ekari moja.



*Kilimo mseto cha mbaazi na mtama*

### PALIZI

Hakikisha shamba linakuwa safi kwa kupalilia mara kwa mara katika wiki 6 za mwanzo. Baada ya hapo palilia tu inapohitajika kufanya hivyo.

### UDHIBITI WA WADUDU WAHARIBIFU

Mbaazi za muda wa kati hushambuliwa kiasi na wadudu. Kama kutajitokeza wadudu wakati wa kutoa maua na wakati wa kujaza vitumba, nyunyizia viuwadudu mara tatu kila baada ya siku 15. viuwadudu vinavyofaa ni: Karate, Amerate, Profecron, COLT (chlorpyrifosi), au vingine utakayoshauriwa na mtaalam.

Scanned with CamScanner